

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA  
MICHEZO

## BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA



### TAARIFA KUHUSU UCHAGUZI WA VIONGOZI WA CHAMA CHA MABONDIA WA NGUMI ZA KULIPWA TANZANIA (TPBA)

**TAREHE: 26 MEI, 2026 DAR ES SALAAM**

Baraza la Michezo la Taifa (BMT) linapenda kuwataarifu wanachama wa Chama cha Mabondia wa Ngumi za Kulipwa Tanzania (Tanzania Professional Boxers Association-TPBA) kuwa, uchaguzi wa Viongozi wa chama hicho utafanyika tarehe **17 Juni, 2026**, ukumbi wa Uwanja wa Benjamin Mkapa uliopo Jijini Dar es Salaam ambapo utatanguliwa na usaili wa wagombea hao tarehe **16 Juni, 2026**.

Kwa mujibu wa Katiba ya TPBA, uchaguzi huo unaratibiwa na kusimamiwa na Kamati Maalum ya Uchaguzi ya BMT. Hivyo, fomu za kuomba nafasi mbalimbali za uongozi zinapatikana ofisi za BMT zilizopo Jijini Dar es Salaam au kupitia tovuti [www.bmt.go.tz](http://www.bmt.go.tz) na msimbopapo (QR Code) kuanzia leo tarehe 26 Mei, 2026. Mwisho wa kuchukua na kurudisha fomu hizo ni tarehe 15 Juni, 2026 saa 09:30 alasiri.

Nafasi za uongozi zinazoombwa, idadi ipo kwenye mabano na ada ya maombi ni Tshs. 200,000 kwa Mwenyekiti (1), Makamu Mwenyekiti (1), Katibu (1), Mweka Hazina (1) na Wajumbe (4) ni Tshs. 50,000. Malipo ya fomu yatafanyika kupitia namba ya malipo ya Serikali **994930024769**.

#### **Sifa za Wagombea;**

1. Awe raia wa Tanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 hadi 60
2. Mgombea nafasi ya Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu na Mweka Hazina awe na kiwango cha elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea
3. Nafasi ya wajumbe, mgombea lazima awe na elimu kuanzia darasa la saba na kuendelea
4. Awe Bondia hai na aliyeorodheshwa katika Box Rec.
5. Awe na leseni ya Bondia wa Ngumi za Kulipwa kutoka mamlaka inayotambulika
6. Awe na nidhamu na hajawahi kukutwa na kosa la jinai

Unaweza kuwasiliana nasi kupitia namba **0767044022** ili kupata ufafanuzi zaidi.

Imetolewa na;

Aminiel Aligaesha

**MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO NA  
UHUSIANO KWA UMMA  
BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA**

